

Upokeaji wa malalamiko kutoka kwa wateja wetu

Mpendwa Mteja,

Benki ya Equity tumejipanga kuhakikisha kunakuwa na urahisi katika upokeaji wa malalamiko kupitia utaratibu wa haraka uliyowekwa katika idara na vitengo vyote ndani ya benki yetu ili kuhakikisha kuwa sera za huduma zetu zinaenda kwa wakati uliopangwa.

Endapo wateja na wadau wetu mtakuwa na malalamiko yoyote kuhusu huduma zetu tunaomba muwasilishe moja kwa moja kwa njia zifuatazo:



Waweza onana na uongozi wa tawi popote pale tulipo nchini
Waweza kujaza fomu maalumu ya malalamiko inayopatikana katika matawi yetu yote kote nchini,



Waweza pia toa malalamiko kupitia kurusa zetu za mitandao ya kijamii



Kutupigia simu kupitia huduma kwa wateja namba **0768985555 / 0768985500**



Kupitia barua pepe; **customercaretz@equitybank.co.tz** au **infotz@equitybank.co.tz**



Waweza pia kufika makao makuu yetu yaliyopo Mtaa wa Ohio, Jengo la Golden Jubilee ghorofa ya tatu



Endapo, kama mteja utaendelea kutoridhishwa na huduma uliyopokea, una haki ya kuwasiliana na Benki Kuu ya Tanzania kupitia dawati la malalamiko. Dawati hili lilianzishwa ili kusaidia kutatua migogoro inayojitokeza kati ya benki na wateja wake.

Malalamiko yako yatapokelewa dawati ya malalamiko kuanzia saa 3 asubuhi hadi saa 6:30 mchana (Jumatatu mpaka Ijumaa)

Jinsi ya kuwasilisha malalamiko yako;

Waweza wasilisha malalamiko yako kupitia njia zifuatazo;

- Kwa mkono Benki Kuu Ya Tanzania - Makao Makuu, Mtaa wa 2 Mirambo, Dar Es Salaam.
- Kwa barua kupitia ofisi ya Katibu wa Benki , S.L.P 2939, Dar es salaam.
- Kwa barua pepe: **complaints-desk@bot.go.tz**
- Kwa faksi: **+255 22 2234067**
- Kwa simu: **+255 22 2233265 / +255 22 2233246**